

## **SUBIRA**

Y. Ulenge

- |    |                                                                                         |     |                                                                                           |
|----|-----------------------------------------------------------------------------------------|-----|-------------------------------------------------------------------------------------------|
| 1. | Subira ina mashaka<br>Hupati kitu haraka<br>Hata kama unataka<br>Huna budi kungojea.    | 9.  | Bali kuna mau.nivu<br>Uwe na uvumilivu<br>Kibichi kiwe kibivu<br>Ukipandacho kukua.       |
| 2. | Utakaa usumbuke,<br>Na wengine wakucheke<br>Mawazo yatapanyike<br>Fikira zimepotea.     | 10. | Vingine ni vya ajabu<br>Vinaishi kama bubu<br>Vikakuwa taratibu<br>Mpaka vimetokea.       |
| 3. | Kila siku, "Nitapata"<br>Wenzako wanakupita,<br>Huishiwi na matata,<br>Hujui kuyatatua. | 11. | Vikuavyo kwa rehema<br>Tumboni mwa kina mama<br>Uvingoje kwa lazima<br>Iwe vya kuhudumia. |
| 4. | Ukikaa hufuruki,<br>Roho yako ina chuki,<br>Maana hujamiliki,<br>Umekaa wangojea.       | 12. | Navyo havina haraka<br>Uvisubiri kwa miaka<br>Kila siku heka.eka<br>Wewe unangojelea.     |
| 5. | Kibichi ukisubiri<br>Unangoja kinawiri<br>Kibivu kina hatari<br>Mara kitajiozea.        | 13. | Nawe unavisubiri<br>Vipate kukusitiri<br>Wewe bado unakiri<br>Mwenyewe wavumilia.         |
| 6. | Lakini imehimizwa<br>Subira kutekelezwa<br>Imani yako hukuzwa<br>Ikiwa umeridhia.       | 14. | Hayo madhila mazito<br>Yakutia roho joto<br>Ikawa una fukuto<br>Na machozi ukalia.        |
| 7. | Ukapata mahitaji<br>Yale unayotaraji<br>Mungu akakufariji<br>Ikawa washangilia.         | 15. | Ukawaza ole wangu<br>Sipati hata wenzangu<br>Ndugu na watoto wangu<br>Wameacha kur.ijia.  |
| 8. | Mwenyewe umeridhika<br>Na kicheko ukacheke<br>Ukasahau mashaka<br>Yaliyokukupatia.      | 16. | Subira ina uzito,<br>Na kutia roho joto,<br>Ukakumbuka uzito,<br>Fahamu zikapotea.        |

17. Ukisubiri mauti,  
Nayo yapo kwa wakati  
Mfano wa kizingiti  
Hayaachi kukujia.
18. Tamaa hutangulia,  
Nawe unajipangia  
Mauti huufukia  
Nyuma na kuvamia.
19. Lakini utafakuri  
Kila unaposubiri  
Kuna mengine ya siri,  
Pengine hukutokea.
20. Ninaombwa jibu lako,  
Kujua mawazo yako,  
Nitulize sikitiko,  
Labda nitatulia.